

Mwl. Samwel Mkumbo

UPONYAJI WA MAJERAHA
YA NDANI.



Mwl. Samwel Mkumbo



+255 764 190 790



Mwl. Samwel Mkumbo



Mwl. Samwel Mkumbo



mkumbo.nuruministry

UPONYAJI WA MAJERAHA YA NDANI.

- ◎ UFAHAMU/MAARIFA JUU YA KUSHUGHULIKIA UPONYAJI WA MAJERAHA YA NDANI.

Utangulizi:

- Maisha ya mwanadamu yamezungukwa na mambo mengi sana ambayo husababisha mtu kwa namna moja ama nyingine **kujikuta amepata maumivu au majeraha ya ndani** au kwa lugha nyingine **majeraha ya nafsi au moyo.**

- Migogoro ya mahusiano, ndoa, hali ya maisha, asili ya mazingira aliyokulia mtu mambo aliyotenda na kutendewa katika maisha na wakati mwingine tukio la mara moja lililotokea na kumfanya mtu ajikute katika hali ya kuwa na majeraha.

- Na sasa hatari kubwa iliyopo ni kwamba hali ya namna hii isipopatiwa uponyaji na kushughulikiwa na kwa namna unavyostahili husababisha athari hata kwa watu wengine ukiacha tu ile kujidhihirisha kwenye maisha ya muhusika moja kwa moja.

◎ **Waebrania 12:15** inasema hivi;

15 mkiangalia sana mtu asiipungukie neema ya Mungu; shina la uchungu lisije likachipuka na kuwasumbua, na watu wengi wakatiwa unajisi kwa hilo.

- Ukisoma mstari huo utaona majeraha ya ndani huwa yana mwanzo wake na yanaweza kutokea mahali ambapo hayakuwepo kutokana na sababu mbalimbali.

- ◎ Ndio maana maandiko yanasema **“shina la Uchungu lisije LIKACHIPUA”** anaposema lisije “likachipua” maana yake halikuwepo kwanza hilo shida na pia kama linaweza kuchipua basi **linaweza kupandwa** na kama **“linaweza kupandwa”** basi pia **linaweza kung’olewa”**.

Hoja ya kwanza:

- Majeraha au maumivu ya ndani ni jambo halisi na linatokea katika maisha yetu ya kila siku na hivyo uponyaji wa ndani ni jambo ambalo ni muhimu tujifunze na kulijua.

- Kwa hiyo ni vema kuangalia kwanza hoja hii tupate kwa sehemu kutazama uwepo wa watu wa(tu) wanaopitia maumivu au majeraha ya ndani na tuangalie na maandiko yanasemaje juu ya jambo hili kisha itatupa nguvu kusogea katika hoja nyingine.

● Isaya 38:12-17 tunasoma hivi;

¹² Kao langu limeondolewa kabisa, limechukuliwa kama hema ya mchungaji; Nimekunja maisha yangu kama mfumaji; atanikatilia mbali na kitanda cha mfumi; Tangu mchana hata usiku wanimaliza. ¹³ **Nalijituliza hata asubuhi; kama simba, aivunja mifupa yangu yote; Tangu mchana hata usiku wanimaliza.** ¹⁴ Kama mbayuwayu au korongo ndivyo nilivyolia; Naliomboleza kama hua; macho yangu yamedhoofu kwa kutazama juu; Ee Bwana, nimeonewa, na uwe mdhamini wangu. ¹⁵

- ◎ Niseme nini? Yeye amenena nami, na yeye mwenyewe ametenda hayo; **Nitakwenda polepole miaka yangu yote, kwa sababu ya uchungu wa nafsi yangu.** ¹⁶ Ee Bwana, kwa mambo hayo watu huishi; Na uhai wa roho yangu u katika hayo yote; Kwa hiyo uniponye na kunihuisha. ¹⁷ Tazama; nalikuwa na uchungu mwingi kwa ajili ya amani yangu; Lakini kwa kunipenda umeniokoa na shimo la uharibifu; Kwa maana umezitupa dhambi zangu zote nyuma yako

- Ukisoma mistari kwa sehemu utaanza kuona suala tinalolitazama hapa kuhusu maumivu au majeraha ya ndani ambao kwenye mistari hii wametumia pia neno **“Uchungu”** ikiwa na maana ileile ya maumivu ya ndani au maumivu ya nafsi.

Tafakari juu ya Maumivu ya ndani.

- Tafakari juu ya mke wa Potifa ni nini anajisikia na anahisi siku Yusufu anasimikwa ramsi kuwa kiongozi wa pili baada ya Farao pale Misri huku akijua kabisa kuwa ile kesi ya kujaribu Kubaka alimsingizia.

- Mfikirie na Yusufu pia ambaye anajiona kabisa anaingia Gerezani kwa kesi ambayo hakufanya halafu ukizingatia anayemhukumu ni Potifa wakati kimsingi amejitahidi kumtunzia ndoa na heshima yake.

- Hebu kaa kwenye nafasi ya watoto wa Yakobo haswa Reubeni ambao wamemuza ndugu yao halafu wakitengeneza mazingira ya kutaka baba yao aamini kuwa Yusufu amekufa na wanamwona kabisa baba yao Analia na kuomboleza juu ya ndugu yao halafu wao wanatumia hela ya biashara ya utumwa kwa kumuza ndugu yao hapo ndo utaelewa namna mioyo inapiga kelele, nafsi zinaumia, kuna namna mambo hayaendi ipasavyo na ni ndani kwa ndani

◎ **Mwanzo 30:1-16** tuone jambo kidogo;

¹ Naye Raheli alipoona ya kuwa hamzalii Yakobo mwana, Raheli alimwonea ndugu yake wivu. Akamwambia Yakobo, Nipe wana; kama sivyo, nitakufa mimi. ² Yakobo akamghadhibikia Raheli, akasema, Je! Mimi ni badala ya Mungu, aliyekuzuilia uzao wa mimba? ³ Akasema, Yuko mjakazi wangu, Bilha, uingie kwake ili kwamba azae juu ya magoti yangu, nami nipate uzao kwa yeye. ⁴ Basi akampa Bilha mjakazi wake kuwa mkewe. Yakobo akaingia kwake. ⁵ Naye Bilha akapata mimba, akamzalia Yakobo mwana.

- 6 Raheli akasema, Mungu amenipa haki yangu, naye amesikia sauti yangu, akanipa mwana. Kwa hiyo akamwita jina lake Dani. 7 Bilha, mjakazi wa Raheli, akapata mimba tena, akamzalia Yakobo mwana wa pili. 8 Raheli akasema, Kwa mashindano makuu nimeshindana na ndugu yangu, nikashinda. Akamwita jina lake Naftali. 9 Lea alipoona ya kuwa ameacha kuzaa, alimtwaa Zilpa, mjakazi wake, akampa Yakobo kuwa mkewe. 10 Zilpa, mjakazi wa Lea, akamzalia Yakobo mwana. 11 Lea akasema, Bahati njema! Akamwita jina lake Gadi.

- 12 Zilpa, mjakazi wa Lea, akamzalia Yakobo mwana wa pili. 13 Lea akasema, Ni heri mimi, maana wanawake wataniita heri. Akamwita jina lake Asheri. 14 Reubeni akaenda siku za mavuno ya ngano akaona tunguja kondeni, akazileta kwa Lea mamaye. Ndipo Raheli akamwambia Lea, Nipe mimi baadhi ya tunguja za mwanao. 15 Naye akamwambia, Je! Ni jambo dogo kuninyang'anya mume wangu; hata wataka kuzitwaa tunguja za mwanangu pia? Raheli akamwambia, Kwa hiyo atalala kwako usiku huu kwa tunguja za mwanao. 16 Yakobo akaja kutoka kondeni jioni, Lea akatoka kumlaki, akasema, Lazima uje kwangu, kwa sababu nimekuajiri, kwa tunguja za mwanangu; akalala kwake usiku ule.

- Nimeweka mistari hiyo natamani tuiangalie hii familia ya Yakobo yenye wake wawili ambao ni ndugu lakini haswa nilitaka tumwangalie Raheli ambae ndiye kipenzi cha Yakobo na aliyekuwa kusudio lake awe mke wake kwa mahari ya kufanya kazi miaka saba.

- ◎ “¹ Naye Raheli alipoona ya kuwa hamzalii Yakobo mwana, Raheli alimwonea ndugu yake wivu. Akamwambia Yakobo, Nipe wana; kama sivyo, nitakufa mimi.....” sasa hayo ni maneno yanayosemwa na mtu aliyekuwa na maumivu ndani ya msongo wa mawazo na huzuni ya moyo na nafsi iliyojeruhika.

- Na hili mpaka leo wanawake wengi wanapitia, huwa wakiwa na changamoto na msongo wa mawazo na huzuni na maumivu ya ndani wanaweza kuongea na kuwaambia waume zao mambo ambayo yanaweza hata kuleta shida kwenye ndoa zao au katika saikolojia za waume zao au marafiki zao.

- Halafu angalia tena hapa ¹⁴ **Reubeni akaenda siku za mavuno ya ngano akaona tunguja kondeni, akazileta kwa Lea mamaye. Ndipo Raheli akamwambia Lea, Nipe mimi baadhi ya tunguja za mwanao. ¹⁵ Naye akamwambia, Je! Ni jambo dogo kuninyang'anya mume wangu; hata wataka kuzitwaa tunguja za mwanangu pia? Raheli akamwambia, Kwa hiyo atalala kwako usiku huu kwa tunguja za mwanao.....**

- Hali ya namna hii iliwahi kumkuta Ayubu wakati marafiki zake walipomtembelea kwa lengo la kumfariji na badala yake walinyamaza kimya, yeye alipofungua kinywa kuanza kunena ukisikiliza maneno aliyokuwa anaongea ndipo utaelewa maana halisi ya maumivu ya ndani.

- Ayubu 2:11-13 imeandikwa hivi;
- ¹¹ Basi ikawa hao rafikize Ayubu watatu walipopata habari ya mabaya hayo yote yaliyomfikilia, wakaja kila mtu kutoka mahali pake; nao ni Elifazi Mtemani, na Bildadi Mshuhi, na Sofari Mnaamathi; wakapatana pamoja ili waende kumlilia Ayubu na kumtuliza moyo. ¹²

- **Basi walipovua macho yao, nao wakali mbali, wasimtambue, wakainua sauti zao na kulia; kila mmoja akararua joho yake, wakarusha mavumbi juu ya vichwa vyao kuelekea mbinguni. ¹³ Kisha wakaketi nchi pamoja naye muda wa siku saba, mchana na usiku, wala hapana mmoja aliyenena naye neno lo lote; kwa maana waliona ya kuwa mashaka yake aliyo nayo ni makuu mno.**

● unganisha na Ayubu 3:1-11 tunasoma;

¹ Baada ya hayo Ayubu akafunua kinywa chake, na kuilaani siku yake. ² Ayubu akajibu, na kusema; ³ Na ipotelee mbali ile siku niliyozaliwa mimi, Na ule usiku uliosema, Mtoto mume ametungishwa mimba. ⁴ Siku hiyo na iwe giza; Mungu asiiangalie toka juu, Wala mwanga usiiangazie. ⁵ Ishikwe na giza, giza tupu, kuwa yake; Wingu na likae juu yake; Chote kiifanyacho siku kuwa giza na kiitishe.

- 6 Tena usiku huo, na ushikwe na giza kuu; Usihesabiwe katika siku za mwaka; Wala kutiwa katika hesabu ya miezi. 7 Tazama, usiku huo na uwe tasa; Wala isiwe ndani yake sauti ya shangwe. 8 Na waulaani hao waulaanio mchana, Hao walio tayari kumwamsha huyo lewiathani. 9 Nyota za mapambazuko yake na ziwe giza; Na utafute mwanga lakini usiupate; Wala usiyaone makope ya asubuhi; 10 Kwa sababu haukuifunga milango ya tumbo la mamangu. Wala kunifichia taabu machoni. 11 Mbona si kufa mimi tokea mimbani? Mbona nisitoe roho hapo nilipotoka tumboni?

- Ukishaona maneno ya namna hii huyu mtu ujue kabisa hayuko sawa katika nafsi yake au kwa lugha nyingine ujue ana maumivu ya ndani ambayo hayajaponywa, lakini maandiko pia yanatuonesha kuwa shida ile ilitokana na wale waliokuja kwake kwa ajili ya kumtuliza moyo au kwa lugha nyingi kumuondolea majeraha yake kushindwa kabisa kufanya kile walichotakiwa kufanya kwa Ayubu

- ⦿ Nisikilize mpendwa wangu ni rahisi sana kuchukulia kawaida unaposikia mtu ana majeraha au maumivu ya ndani lakini hili si jambo la kawaida kabisa kwenye maisha ya mwanadamu, nakumbuka moyo wa mtu haujatengenezwa kubeba machungu au maumivu ndani yake.
- ⦿ Ukisikia mtu amepata msiba au jambo ambalo limesababisha apate maumivu ndani yake usilichukulie kirahisi jambo hilo hata kidogo maana maumivu ndani ya mtu ni jambo linaloweza kufunua mambo mengi sana ndani ya huyo mtu kwa namna ambayo usingeweza kujua kama ndani yake kuko hivyo.

Hoja ya Pili:

- ◎ Ni mapenzi/mpango wa Mungu watu wake wapate uponyaji wa ndani na waondokane na maumivu ya ndani.

- Ni furaha sana kujua kwamba unachokishughulikia au kutaka kukifanya au ufanyiwe ni mapenzi ya Mungu kwenye maisha yako, hii inakupa ujasiri sana wa kufanya jambo au hata kama ni maombi inakupa nguvu ya kuomba ipasavyo.

● **1 Yohana 5:14-15** maandiko yanasema;

¹⁴ Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia. ¹⁵ Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba.

- Kwa hiyo basi kama tuna uhakika kupata uponyaji wa ndani ni mapenzi ya Mungu basi tuna uhakika wa kujibiwa na kupata uponyaji sawa na tunavyohitaji.

● **Isaya 30:18-26** maandiko yanasema hivi;

18 Kwa ajili ya hayo Bwana atangoja, ili awaonee huruma, na kwa ajili ya hayo atatukuzwa, ili awarehemu; kwa maana Bwana ni Mungu wa hukumu; heri wote wamngojao. ¹⁹ Kwa maana watu watakaa katika Sayuni huko Yerusalemu; wewe hutalia tena; hakika yake atakuonea rehema nyingi kwa sauti ya kilio chako; asikiapo ndipo atakapokujibu.

- 20 Na ingawa Bwana atawapeni chakula cha shida na maji ya msiba, lakini waalimu wako hawatafichwa tena, ila macho yako yatawaona waalimu wako; 21 na masikio yako yatasikia neno nyuma yako, likisema, Njia ni hii, ifuateni; mgeukapo kwenda mkono wa kulia, na mgeukapo kwenda mkono wa kushoto. 22 Nanyi mtakitia najisi kifuniko cha sanamu zenu za fedha zilizochongwa, na mabamba ya sanamu zenu za dhahabu zilizoyeyushwa; utazitupilia mbali kama kitu kilicho najisi; utasema, Haya, toka hapa.

- 23 Naye atatoa mvua juu ya mbegu zako, upate kuipanda nchi hii; na mkate wa mazao ya nchi, nayo itasitawi na kuzaa tele; katika siku hiyo ng'ombe zako watakula katika malisho mapana. 24 Ng'ombe pia na wana-punda wailimao nchi watakula chakula kilichokolea, kilichopepetwa kwa ungo na kwa pepeo. 25 Na juu ya kila mlima mrefu, na juu ya kila kilima kilichoinuka, itakuwapo mito na vijito vya maji, katika siku ya machinjo makuu itakapoanguka minara.

- 26 Na tena nuru ya mwezi itakuwa kama nuru ya jua, na nuru ya jua itaongezeka mara saba, kama nuru ya siku saba, katika siku ile Bwana atakapofunga mapigo ya watu wake, na kuliponya pigo la jeraha yao.

- Maandiko yanatuonesha ya kwamba Bwana mwenyewe atafanya jambo kwa ajili ya wana wa Israeli (*kwa sasa tuite ni waliokoka/wakristo*) la kuwaponya majeraha yao na kuwaondolea maumivu yao katika maisha na kuwapa tumaini jipya.

◎ Yeremia 30:12-17 tunasoma hivi;

12 Maana Bwana asema hivi, Maumivu yako hayaponyekani, na jeraha yako ni kubwa. ¹³ Hapana mtu wa kukutetea; kwa jeraha yako huna dawa ziponyazo. ¹⁴ **Wote wakupendao wamekusahau; hawakutafuti;** maana nimekujeruhi kwa jeraha ya adui, kwa adhabu ya mtu mkatili; kwa sababu ya ukubwa wa uovu wako, kwa sababu dhambi zako zilikuwa zimeongezeka.

**15 Mbona unalilia maumivu yako?
Hayaponyeki maumivu yako; kwa
sababu ya ukubwa wa uovu wako, kwa
sababu dhambi zako zimeongezeka,
nimekutenda haya. ¹⁶ Basi, watu wote
wakulao wataliwa; na adui zako wote
watakwenda kufungwa; kila mmoja wao;
na hao waliokuteka nyara watatekwa; na
wote waliokuwinda nitawafanya kuwa
mawindo.**

17 Maana nitakurudishia afya, nami nitakuponya jeraha zako, asema Bwana, kwa sababu wamekuita, mwenye kutupwa, wakisema, Ni Sayuni, ambao hapana mtu autakaye.

⦿ **Zaburi 147:1-3** maandiko yanasema;

¹ Haleluya. Msifuni Bwana; Maana ni vema kumwimbia Mungu wetu, Maana kwapendeza, kusifu ni kuzuri. ² Bwana ndiye aijengaye Yerusalemu, Huwakusanya waliotawanyika wa Israeli. ³ Huwaponya waliopondeka moyo, Na kuziganga jeraha zao.

- Mstari wa 3 ndio niliokuwa nauwinda katika maandiko hayo maana umebeba maana kubwa sana katika somo letu, kwamba Mungu mwenyewe huwa anafanya kazi ya **“kuwaponya waliopondeka moyo”** lakini maandiko pia yanasema haishii hapo huwa **“anaganga jeraha zao”**.

⦿ ***Amplified Bible*** inasema hivi;

*“PRAISE THE Lord! For it is good to sing praises to our God, for He is gracious and lovely; praise is becoming and appropriate. The Lord is building up Jerusalem; He is gathering together the exiles of Israel. He heals the brokenhearted and binds up their wounds **[curing their pains and their sorrows]***

- ◎ Uponyaji wa ndani ni jambo nyeti na kulichukulia umakini mkubwa na kwa kina.

● **2 Wafalme 4:13-28 inasema hivi;**

¹³ Akamwambia, Sema naye sasa, Tazama, wewe umetutunza sana namna hii; utendewe nini basi? Je! Uombewe neno kwa mfalme, au kwa amiri wa jeshi? Yule mwanamke akamjibu, Mimi ninakaa katika watu wangu mwenyewe ¹⁴ Akasema, Basi, atendewe nini? Gehazi akajibu, Hakika hana mwana, na mumewe ni mzee. ¹⁵ Akamwambia, Kamwite. Naye alipokwisha kuitwa, akasimama mlangoni

- **¹⁶ Akasema, Panapo wakati huu mwakani, utamkumbatia mwana. Akasema, La! Bwana wangu, wewe mtu wa Mungu, usiniambie mimi mjakazi wako uongo. ¹⁷ Yule mwanamke akachukua mimba, akazaa mtoto mume wakati uo huo mwakani, kama Elisha alivyomwambia. ¹⁸ Hata yule mtoto alipokua, ikawa siku moja alitoka kwenda kwa baba yake kwenye wavunao. ¹⁹ Akamwambia baba yake, Kichwa changu! Kichwa changu! Naye akamwambia mtumishi wake, Mchukue kwa mama yake.**

- ²⁰ Akamchukua, akampeleka kwa mama yake, naye akakaa magotini mwake hata adhuhuri, kisha akafa. ²¹ Mamaye akapanda juu, akamlaza juu ya kitanda cha yule mtu wa Mungu, akamfungia mlango, akatoka. ²² Kisha akamwita mumewe, akasema, Tafadhali, uniletee mtu mmoja wa watumishi, na punda mmoja, ili nimwendee yule mtu wa Mungu kwa haraka, nikarudi tena. ²³ Akasema, Kwa nini kumwendea leo? Sio mwandamo wa mwezi, wala sabato. Akasema, Si neno.

- 24 Akatandika punda, akamwambia mtumishi wake, Mwendeshe, twendelee mbele. Usinipunguzie mwendo, nisipokuambia. 25 Basi akaenda, akafika kwa yule mtu wa Mungu, katika mlima wa Karmeli. Ikawa, yule mtu wa Mungu alipomwona kwa mbali, akamwambia Gehazi mtumishi wake, Tazama, Mshunami yule kule. 26 Tafadhali piga mbio sasa kwenda kumlaki, ukamwambie, Hujambo? Mume wako hajambo? Mtoto hajambo? Akajibu, Hawajambo.

- 27 Naye alipofika kwa yule mtu wa Mungu kilimani, alimshika miguu. Gehazi akakaribia amwondoe; lakini mtu wa Mungu akamwambia, Mwache; maana roho yake ndani yake ina uchungu; na Bwana amenificha, wala hakuniambia. 28 Yule mwanamke akasema, Je! Naliomba mwana kwa bwana wangu? Mimi sikusema, Usinidanganye?

- *(a) Tatizo la kukosa mtoto liliathiri maisha ya ndani ya huyu mama, au liliathiri moyo wa huyu mama na alikuwa na maumivu ambayo hakutaka mtu mwingine ajue.*

- *(b) Wapo watu ambao wana majeraha au matatizo na hawako tayari au hawawezi kuyasema na wala kuyashughulikia wameamua wakae nayo hata kama akitokea mtu wa kuwasaidia au ukitaka kuwasaidia wanaweza kukukatisha tama ahata kama mambo hayo ni sumu kwenye maisha yao*

- (c) *Usije kumzuia mtu mwenye majeraha ya ndani kuonesha majeraha yake maana itakusaidia kujua namna ya kuyaponya sawa na Ufunuo anaoweza kutoa Mungu kwa wakati husika.*

- *(d) Maumivu au majeraha ya ndani huwa yana tabia ya kutaka kujirudia ikiwa yameshashughulikiwa kwenye maisha yako.*



- Maumivu au majeraha ya ndani
yakizidi sana hali ya mtu inakuwa
mbaya zaidi

- Wakati mwingine maumivu yakizidi sana na majeraha yakiwa makali Zaidi unaweza kujikuta mtu badala ya kusonga mbele anarudi nyuma Zaidi tofauti na alipokuwapo mara ya kwanza haswa kwenye usemi wake na hata Imani yake.

- kwa sehemu kubwa sana majeraha au maumivu yasiyotibiwa au yaliponywa yakarudi tena kwa jinsi ile au kwa jinsi nyingine yakizidi sana hufanya hali ya mtu kuwa mbaya kuliko ile ya kwanza na hata Imani yake au kiwango chake cha kiroho kuathirika kabisa.

- ◎ **Ufunuo 16:1-11** maandiko yanasema;
- ◎ ¹ Nikasikia sauti kuu kutoka hekaluni, ikiwaambia wale malaika saba, Enendeni, mkavimimine vile vitasa saba vya ghadhabu ya Mungu juu ya nchi. ² Akaenda huyo wa kwanza, akakimimina kitasa chake juu ya nchi; pakawa na jipu baya, bovu, juu ya wale watu wenye chapa ya huyo mnyama, na wale wenye kuisujudia sanamu yake. ³ Na huyo wa pili akakimimina kitasa chake juu ya bahari, ikawa damu kama damu ya mfu, na vitu vyote vyenye roho ya uhai katika bahari vikafa. ⁴ Na huyo wa tatu akakimimina kitasa chake juu ya mito na chemchemi za maji; zikawa damu.

- 5 Nami nikamsikia malaika wa maji akisema, Wewe u mwenye haki, uliyeko na uliyekuwako, Mtakatifu, kwa kuwa umehukumu hivi; 6 kwa kuwa walimwaga damu ya watakatifu na ya manabii, nawe umewapa damu wainywe; nao wamestahili. 7 Nikaisikia hiyo madhabahu ikisema, Naam, Bwana Mungu Mwenyezi, ni za kweli, na za haki, hukumu zako. 8 Na huyo wa nne akakimimina kitasa chake juu ya jua, nalo likapewa kuwaunguza wanadamu kwa moto. 9 Wanadamu wakaunguzwa maunguzo makubwa, nao wakalitukana jina la Mungu aliye na mamlaka juu ya mapigo hayo; wala hawakutubu wala kumpa utukufu.

- ④ ¹⁰ Na huyo wa tano akakimimina kitasa chake juu ya kiti cha enzi cha yule mnyama; ufalme wake ukatiwa giza; wakatafuna ndimi zao kwa sababu ya maumivu, ¹¹ wakamtukana Mungu wa mbingu kwa sababu ya maumivu yao, na kwa sababu ya majipu yao; wala hawakuyatubia matendo yao.

- Umeona kilichotokea katika mistari hiyo, nadhani sasa ufahamu wetu hautakuwa wa kawaida kuhusu suala la majeraha au maumivu, kadiri maumivu yao yalivyozidi unaweza kuhisi yamkini wangeweza kumtazama Mungu na kubadilisha maisha yao, lakini haikuwa hivyo kabisa Zaidi sana walizidi kuleta mapigo na maumibu juu ya maisha yao.

- Na ndio maana ni ukweli ulio wazi kwamba adhabu na mapigo na majeraha haijawahi kuwa njia nzuri sana katika kumbadilisha mtu na kumfanya ageuke, na ndio maana Mungu hakuadhibu kwa ghadhabu kila unapokosea maana maumivu na majeraha ya mara kwa mara humfanya mtu kuharibika Zaidi kwenye eneo alilopo.

- Fuatilia asilimia kubwa ya watoto ambao walichapwa au kuadhibiwa pasipo kiasi walipokuwa wadogo unakuta wengi wamekuwa wabaya zaid ya zamani kwa sababu maumivu ni ngumu sana kumbadilisha mtu maana yakizidi sana huleta madhara Zaidi.

- Hivyo basi:

- *Unaweza kuelewa kwa undani ninaposema ni mapenzi ya Mungu sisi tuponywe na maumivu na majeraha ya ndani maana kama yasiposhughulikiwa huleta shida na husumbua Zaidi na Zaidi katika maisha yetu ya kila siku.*

- ◎ Kwanini Mungu anataka watoto wake wapate uponyaji kamili na wa kwelikweli juu ya maumivu yao ya ndani?

- Hili ni swali muhimu katika hoja hii ya pili ya somo letu maana inafunua kwa undani sasa na kutupa mwanga kuona hilo tunalolisema kwamba ni mapenzi ya Mungu watoto wake waponywe na wawe huru kutokana na maumivu ya ndani, lakini swali ni kwanini Mungu anataka watu wake au watoto wake wapate uponyaji wa ndani.

- Si jambo rahisi mwanadamu kushughulika na uponyaji wa ndani aidha kwake mwenyewe au kwa mtu mwingine bila ya Neema ya Mungu maana mwanadamu akijitahidi mwenyewe basi utakuwa ni uponyaji wa juu juu tu.

- Si jambo rahisi mwanadamu kushughulika na uponyaji wa ndani aidha kwake mwenyewe au kwa mtu mwingine bila ya Neema ya Mungu maana mwanadamu akijitahidi mwenyewe basi utakuwa ni uponyaji wa juu juu tu.

- Kimsingi kama mwanadamu akijitahidi kushughulika na suala la uponyaji wa ndani atafanya kwa juu juu maana haya mambo ni rohoni sana, na ndio maana Mungu mwenyewe anaamua kuingilia hapo na kukaa hapo.

- Mungu hataki uponyaji wa juu juu huku watu wakibaki na hali mbaya na tena ni mbaya Zaidi kwa sababu ni mambo yanayowasumbua ndani, yaani misongo ya mawazo, hasira, chuki, vinyongo na hata mioyo iliyojaa visasi vya kila namna na uchungu usiotazamika.

- Yeremia 6:14-16 maandiko yanasema hivi;
- ¹⁴ Wameiponya jeraha ya watu wangu kwa juu juu tu, wakisema, Amani, Amani, wala hapana amani. ¹⁵ Je! Walitahayarika, walipokuwa wameunda machukizo? La, hawakutahayarika hata kidogo, wala hawakuweza kuona haya usoni; basi, wataanguka miongoni mwa hao waangukao; wakati nitakapowajilia wataangushwa chini, asema Bwana.

- ¹⁶ Bwana asema hivi, Simameni katika njia kuu, mkaone, mkaulize habari za mapito ya zamani, I wapi njia iliyo njema? Mkaende katika njia hiyo, nanyi mtajipatia raha katika nafsi zenu. Lakini walisema, Hatutaki kwenda katika njia hiyo.

- Kuna mambo kama mawili nilitamani uyaone hapo kwenye hiyo mistari kwa haraka na kwa ufupi tu maana tutayatazama kwa undani kidogo huko mbele kadiri tunavyojifunza lakini katika hoja hii tutazame kidogo tu;

- *Mungu anataka tujue kwamba kama tunajishughulisha na uponyaji wa watu basi ni vema tukafanya kwa uhakika na sio juu juu tu, tena hakuna jambo baya kama kuwapa watu tumaini katika mazingira ambayo wanabaki na vifungo na shida haswa za ndani wakati Mungu anataka watu wafunguliwe kwelikweli.*

- Kuna hii changamoto ya kuona watu wana shida lakini aidha kwa kushindwa au kuogopa au kuona wanaweza wasituelewe basi tunawatia moyo halafu tunataka wawe na Amani na furaha wawe na hali ya kawaida wakati kimsingi Mungu anataka watu wafunguliwe na wawe huru kwelikweli.

- Unaposhughulika na tatizo la mtu haswa lile la ndani ni muhimu kujua kuwa inahitajika umakini na utayari wa mtu kuwa huru, lakini hata wewe nwenyewe ambaye una jambo linalokutesa ndani yako ni vema kujua kuwa usichoke na kukata tamaa pale unaposhughulika na jambo la ndani.

- Mungu anawaambia kwamba ¹⁴
**Wameiponya jeraha ya watu wangu
kwa juu juu tu, wakisema, Amani,
Amani, wala hapana amani.....**
- Hii ni mbaya sana, tatizo la mtu ambalo
lipo ndani likiacha ni heri, na
likiondolewa kabisa ni heri mara elfu elfu
lakini likiguswa juu juu na kisha
likaachwa ni hatari mara elfu nyingi pia.

- ◎ Iko hivi;
- ◎ Ikiwa kuna jambo linakuumiza ndani yako na limezalisha ugonjwa wa ndani basi USIKUBALI FARAJA tafuta UPONYAJI.

- ◎ **1 Samweli 1:1-18** maandiko yanasema hivi;
- ◎ **¹ Palikuwa na mtu mmoja wa Rama, Msufi, wa nchi ya milima milima ya Efraimu, jina lake akiitwa Elkana, mwana wa Yerohamu, mwana wa Elihu, mwana wa Tohu, mwana wa Sufu, Mwefraimu ² naye alikuwa na wake wawili; jina lake mmoja akiitwa Hana, na jina lake wa pili aliitwa Penina; naye huyo Penina alikuwa na watoto, lakini Hana hakuwa na watoto.**

- ③ **Na mtu huyo alikuwa akikwea kutoka mjini kwake mwaka kwa mwaka, ili kuabudu, na kumtolea Bwana wa majeshi dhabihu katika Shilo. Na wale wana wawili wa Eli, Hofni na Finehasi, makuhani wa Bwana, walikuwako huko.**

- ④ ⁴ Hata siku ile ilipofika Elkana alipotoa dhabihu, kumpa mkewe Penina sehemu, akawapa na watoto wake wote, waume kwa wake, sehemu zao; ⁵ lakini Hana humpa sehemu mara mbili; maana alimpenda Hana, ingawa Bwana alikuwa amemfunga tumbo. ⁶ Ila mwenzake humchokoza sana, hata kumsikitisha, kwa sababu Bwana alikuwa amemfunga tumbo.

- 7 Tena mumewe akafanya hivyo mwaka kwa mwaka, hapo yule mwanamke alipokwea kwenda nyumbani kwa Bwana, ndivyo yule alivyomchokoza; basi, kwa hiyo, yeye akalia, asile chakula

- 8 Elkana mumewe akamwambia, Hana, unalilia nini? Kwani huli chakula? Kwa nini moyo wako una huzuni? Je! Mimi si bora kwako kuliko watoto kumi? 9 Ndipo Hana akainuka, walipokwisha kula na kunywa huko Shilo. Naye Eli, kuhani, alikuwa akiketi kitini pake penye mwimo wa hekalu la Bwana. 10 Naye huyo mwanamke alikuwa na uchungu rohani mwake, akamwomba Bwana akalia sana.

- © 11 Akaweka nadhiri, akasema, Ee Bwana wa majeshi, ikiwa wewe utaliangalia teso la mjakazi wako, na kunikumbuka, wala usinisahau mimi mjakazi wako, na kunipa mimi mjakazi wako mtoto mume, ndipo mimi nitakapompa Bwana huyo mtoto siku zote za maisha yake, wala wembe hautamfikilia kichwani kamwe.

- **¹² Ikawa, hapo alipodumu kuomba mbele za Bwana, Eli akamwangalia kinywa chake. ¹³ Basi Hana alikuwa akinena moyoni mwake; midomo yake tu ilionekana kama anena, sauti yake isisikiwe; kwa hiyo huyo Eli alimdhania kuwa amelewa. ¹⁴ Ndipo Eli akamwambia, Je! Utakuwa mlevi hata lini? Achilia mbali divai yako.**

- ◎ **15 Hana akajibu, akasema, Hasha! Bwana wangu, mimi ni mwanamke mwenye roho ya huzuni, mimi sikunywa divai wala kileo, ila nimeimimina roho yangu mbele za Bwana. 16 Usimdhanie mjakazi wako kuwa ni mwanamke asiyefaa kitu; kwa kuwa katika wingi wa kuugua kwangu na kusikitika kwangu ndivyo nilivyonena hata sasa.**

- 17 Ndipo Eli akajibu, akasema, Enenda kwa amani; na Mungu wa Israeli akujalie haja yako uliyomwomba. 18 Naye akasema, Mjakazi wako na aone kibali machoni pako. Basi huyo mwanamke akaenda zake, naye akala chakula, wala uso wake haukukunjamana tena.

- Katika maandiko hayo unaweza kujifunza kitu kupitia hana ya kwamba japokuwa mume wake Elkana alimtia moyo na kumpa faraja yeye hakuridhika na kuponywa kwa juujuu tu, hakuridhika na kuambiwa maneno ya kumtia moyo wakati majeraha yake na uchungu na huzuni na msongo wa mawazo alionao havijatoka bado ndani yake, ...

- ◎ ...hakuridhika na maneno ya kuambiwa wakati anajua kuna kicheko cha Penina kila mwaka na kila mara alirudi kwenye madhabahu kuendelea kusema na BWANA ili yamkini apate uponyaji wa kweli kweli.

- ② 2. Mara nyingi watu wenye majeraha na maumivu ya ndani huwa ni changamoto sana kuwa na uwezo mzuri wa kusikiliza.

- Uwezo wa kusikiliza wa mwanadamu na kukubali na kuelewa huwa unapungua kadiri anavyokuwa na maumivu, hii ni kwa maumivu ya nje na hata ya ndani. Mtu mwenye maumivu na uchungu na majeraha ya ndani huwa anapoteza uwezo wa kusikiliza na kufanya maamuzi hata kama atapewa ushauri mzuri kabisa lakini hawezi kusikiliza kirahisi kwa sababu ndani yake ana uchungu na ana maumivu ya kutosha sana.

- Angalia maandiko yanachosema kwenye ile Yeremia tuliyosema hapo juu, utaona maneno haya juu ya hao watu;
- . ¹⁵ **Je! Walitahayarika, walipokuwa wameunda machukizo? La, hawakutahayarika hata kidogo, wala hawakuweza kuona haya usoni; basi, wataanguka miongoni mwa hao waangukao; wakati nitakapowajilia wataangushwa chini, asema Bwana..**

- 16 Bwana asema hivi, Simameni katika njia kuu, mkaone, mkaulize habari za mapito ya zamani, I wapi njia iliyo njema? Mkaende katika njia hiyo, nanyi mtajipatia raha katika nafsi zenu. Lakini walisema, **HATUTAKI KWENDA KATIKA NJIA HIYO**

- Unaweza kuona namna watu wanavyoweza kuingia katika hali mbaya Zaidi wanapokuwa na majeraha au maumivu ya ndani kwa sababu huwa wanapoteza hali ya kusikiliza au kupokea ushauri haswa ulio mzuri na hii inaingia hadi kwenye makanisa ikiwa ndani ya kanisa kuna watu kadhaa wenye shida ya kuugua ndani na majeraha na maumivu na hawajaponywa, unakuta hata mafundisho yawe mazuri kiasi gani huwa ni ngumu sana kusikia na kuyafanyia kazi.

- *Ni sawa na kusema;*
- **Maumivu au majeraha ya ndani huwa yana tabia ya kuziba masikio ya ndani na mtu hawezi kusikia hata shauri lililo jema linapokuja kwenye maisha yake.**

- Hili jambo unaweza kujifunza kupitia maisha ya mtoto wa kwanza wa Adamu aliyekuwa akiitwa Kaini alijikuta anapata maumivu mpaka anashindwa kusikia sauti na mahusia aliyokuwa anapewa na Mungu.



● **Mwanzo 4:1-13** tunasoma hivi;

● ¹ **Adamu akamjua Hawa mkewe; naye akapata mimba, akamzaa Kaini, akasema, Nimepata mtoto mwanamume kwa Bwana.**
² **Akaongeza akamzaa ndugu yake, Habili. Habili alikuwa mchungu kondoo, na Kaini alikuwa mkulima ardhi.** ³ **Ikawa hatimaye Kaini akaleta mazao ya ardhi, sadaka kwa Bwana.** ⁴ **Habili naye akaleta wazao wa kwanza wa wanyama wake na sehemu zilizonona za wanyama. Bwana akamtakabali Habili na sadaka yake;**

- 5 bali Kaini hakumtakabali, wala sadaka yake. Kaini akaghadhibika sana, uso wake ukakunjamana. 6 Bwana akamwambia Kaini, Kwa nini una ghadhabu? Na kwa nini uso wako umekunjamana? 7 Kama ukitenda vyema, hutapata kibali? Usipotenda vyema dhambi iko, inakuotea mlangoni, nayo inakutamani wewe, walakini yapasa uishinde. 8 Kaini akamwambia Habili nduguye, *Twende uwandani* Ikawa walipokuwapo uwandani, Kaini akamwinukia Habili nduguye, akamwua.

- 9 Bwana akamwambia Kaini, Yuko wapi Habili ndugu yako? Akasema, Sijui, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu? 10 Akasema, Umefanya nini? Sauti ya damu ya ndugu yako inanililia kutoka katika ardhi. 11 Basi sasa, umelaaniwa wewe katika ardhi, iliyofumbua kinywa chake ipokee damu ya ndugu yako kwa mkono wako; 12 utakapoilima ardhi haitakupa mazao yake; utakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani. 13 Kaini akamwambia Bwana, Adhabu yangu imenikulia kubwa, haichukuliki.

- Unaweza kuona sasa yaani kwa maumivu aliyokuwa nayo Kaini hata Mungu alipomhubiria Injili ili abadilike na aache mawazo aliyonayo juu ya ndugu yake lakini haikuwezekana kulifungua sikio la kaini bali alizidi sana kupanga mikakati ya kutekeleza maumivu yake yanavyomwambia.

- Tena Zaidi hata baada ya kumaliza kufanya kile maumivu yalimtuma kufanya aliendelea kuwa na shida ndani ya nafsi yake mwenyewe na kiburi cha hali ya juu.



©⁸ Kaini akamwambia Habili nduguye, *Twende uwandani* Ikawa walipokuwapo uwandani, Kaini akamwinukia Habili nduguye, akamwua.⁹ Bwana akamwambia Kaini, Yuko wapi Habili ndugu yako? Akasema, Sijui, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?.....

- Hebu tafakari hayo majibu ni mtu anamjibu Mungu, lakini utagundua kabisa hiyo ni hasira, wivu uliojengwa ndani na ukatenegeneza maumivu makali sana na kisha kuzalisha mauaji na kiburi ndani ya Kaini. Na mtu wa namna hii si rahisi sana kumbadilisha maisha yake ikiwa

- ◎ Ni kazi ngumu kumhubiri Injili mtu mwenye hasira, mwenye chuki na mwenye msongo wa mawazo au huzuni kali sana au ambaye ana uchungu moyoni mwake, ni kazi ngumu sana kumsaidia mtu wa namna hiyo kwenye maisha yake sababu hali za namna hiyo huwa zinaleta shida ya kutokusikia sauti ya maonyo au hata sauti ya Upendo.



Hoja ya Tatu:

- **Ufahamu sahihi juu ya uponyaji wa ndani huleta uponyaji wa ndani ulio kamili.**
- Kama tulivyotazama katika hoja namba mbili ya kwamba ni mapenzi ya Mungu kuwa watoto wake na wanadamu wawe na hali njema katika utu wao wa ndani na kwamba wakae katika hali ya uzima kuanzia roho zao, nafsi na miili yao.

- ◎ Sasa ili tuweze kuyapokea hayo mapenzi ya Mungu lazima tuwe na ufahamu namna ya kufanya kwenye maisha yetu ili tupate huo uponyaji wa ndani lakini pia kuwasaidia wale wanaopitia hali za maisha zilizotia majeraha ndani ya maisha yao.
- ◎ Ufahamu ni suala muhimu juu ya jambo lolote unalotaka kulishughulikia ikiwa pamoja na majeraha ya ndani.

- ni muhimu kujua kuwa unapotaka kushughulika na jambo lolote lile haswa haya ya rohani na masuala ya uponyaji wa ndani kuwa na ufahamu au kwa lugha nyingine kuwa na maarifa ni jambo muhimu sana.

Hoja ya Tatu:

- Ufahamu sahihi juu ya uponyaji wa ndani huleta uponyaji wa ndani ulio kamili.
- Kama tulivyotazama katika hoja namba mbili ya kwamba ni mapenzi ya Mungu kuwa watoto wake na wanadamu wawe na hali njema katika utu wao wa ndani na kwamba wakae katika hali ya uzima kuanzia roho zao, nafsi na miili yao.

- Sasa ili tuweze kuyapokea hayo mapenzi ya Mungu lazima tuwe na ufahamu namna ya kufanya kwenye maisha yetu ili tupate huo uponyaji wa ndani lakini pia kuwasaidia wale wanaopitia hali za maisha zilizotia majeraha ndani ya maisha yao.

- Ufahamu ni suala muhimu juu ya jambo lolote unalotaka kulishughulikia ikiwa pamoja na majeraha ya ndani
- Ni muhimu kujua kuwa unapotaka kushughulika na jambo lolote lile haswa haya ya rohani na masuala ya uponyaji wa ndani kuwa na ufahamu au kwa lugha nyingine kuwa na maarifa ni jambo muhimu sana.

- Mambo mengi tunashindwa kuyafanya si kwa sababu hayawezekani ila ni kwa sababu hatuna maarifa au ufahamu juu ya mambo hayo kwa hiyo unakuta wengine wanashindwa kuyafanya na wengine wanaweza kuyafanya kwa uhakika kabisa.

- Tofauti kubwa kati ya anayeweza kufanya jambo Fulani na asiyeweza ni kiwango cha ufahamu/maarifa walichonacho ndani yao wakati wanashughulika na jambo hilo. Kwa hiyo ni muhimu sana kutafuta ufahamu kwanza kwenye jambo unalotaka kushughulika nalo, na vivyo hivyo hata kwenye hili la uponyaji wa ndani.

- ◎ Yohana 9:1-12 imeandikwa;
- ◎ ¹ Hata alipokuwa akipita alimwona mtu, kipofu tangu kuzaliwa. ² Wanafunzi wake wakamwuliza wakisema, Rabi, ni yupi aliyetenda dhambi, mtu huyu au wazazi wake, hata azaliwe kipofu? ³ Yesu akajibu, Huyu hakutenda dhambi, wala wazazi wake; bali kazi za Mungu zidhihirishwe ndani yake.

- ④ ⁴ Imetupasa kuzifanya kazi zake yeye aliyenipeleka maadamu ni mchana, usiku waja asipoweza mtu kufanya kazi. ⁵ Muda nilipo ulimwenguni, mimi ni nuru ya ulimwengu. ⁶ Alipokwisha kusema hayo, alitema mate chini, akafanya tope kwa yale mate. Akampaka kipofu tope za macho, ⁷ akamwambia, Nenda kanawe katika birika ya Siloamu, (maana yake, Aliyetumwa). Basi akaenda na kunawa; akarudi anaona.

- Basi jirani zake, na wale waliomwona zamani kuwa ni mwombaji, wakasema, Je! Huyu siye yule aliyekuwa akiketi na kuomba? ⁹ Wengine wakasema, Ndiye. Wengine wakasema, La, lakini amefanana naye. Yeye mwenyewe alisema, Mimi ndiye. ¹⁰ Basi wakamwambia, Macho yako yalifumbuliwaje? ¹¹ Yeye akajibu, Mtu yule aitwaye Yesu alifanya tope, akanipaka macho akaniambia, Nenda Siloamu ukanawe; basi nikaenda na kunawa, nikapata kuona. ¹² Wakamwambia, Yuko wapi huyo? Akasema, Mimi sijui.

- ◎ Sasa katika mistari hiyo kuna mambo kadhaa ambayo yanahusika na masuala ya ufahamu unapotaka kushughulika na tatizo.
- ◎ Kuna mambo ambayo unaweza kujifunza kama haya;

- 1. *Kama wanafunzi wa Yesu wangepewa kazi au nafasi ya kumwombea yule kipofu na kushughulika na tatizo lake basi wangeishia kumwambia Atubu dhambi zake au wangewaita wazazi wake waje kutubu dhambi zao.*

- Maana kwa wao ufahamu waliokuwa nao ni kwamba kwa hali kama ile aliyokuwa nayo huyu kipofu basi inatokana na dhambi aidha za kwake au za wazazi wake kwa hiyo kama wangepewa nafasi basi sala ya toba tu ingehusika kwanza.

- Unaweza kuona sasa, kwa hiyo wao dhambi ndo ilikuwa mtazamo na ufahamu na maarifa pekee waliyonayo juu ya mtu kuzaliwa tangu kipofu, na ndio maana hawakuwa na shida na dhambi walijua lazima ipo wao walichotaka kujua kuwa ni nani sasa aliitenda hiyo dhambi mpaka huyu ndugu kazaliwa kipofu.

- Na unadhani kwamba wangepata matokeo ya hicho wanachoomba? Ni dhahiri kwamba wasingepata maana wangekuwa wanaomba nje kabisa ya kile walichotakiwa kukifanya au kukiomba au kukishughulikia.

- **Tafakari hivi;**

- *Kujibu mtihani sio shida hata kidogo ila shida ni majibu yako kuuwiana na msahishaji wa mtihani maana unaweza kujaza karatasi lakini bado ukafeli hicho ulichojibu.*
- *Vivyo hivyo, kuomba si kazi au kushughulika na majeraha au maumivu ya ndani si kazi ila kazi ni namna unavyoshughulikia ni kwa usahihi au una ufahamu na unachokifanya....*

- 2. *Kuna mambo watu wanapitia ambayo si mazuri sana kwa namna moja ama nyingine lakini yanaweza kuwa msaada mkubwa kama watapata ufahamu sahihi kwanini yamewapata na wayashughulikieje.*

- Hili wazo tunalipata kwa kuangalia namna Yesu alivyowajibu wanafunzi wake juu ya suala la kipofu waliyemwona na kujua kuwa ana hali hiyo tangu kuzaliwa tumboni mwa mama yake, angalia namna alivyowajibu.

- ③ ³ Yesu akajibu, Huyu hakutenda dhambi, wala wazazi wake; bali kazi za Mungu zidhihirishwe ndani yake. ⁴ Imetupasa kuzifanya kazi zake yeye aliyenipeleka maadamu ni mchana, usiku waja asipoweza mtu kufanya kazi. ⁵ Muda nilipo ulimwenguni, mimi ni nuru ya ulimwengu.

- Kimsingi kwa hali ya kawaida kuna mambo ambayo yanatupata na yanaumiza sana na kutesa watu na mengine hata kuwapoteza maana si mazuri lakini kulingana na maandiko katika mambo hayo hayo mabaya na wakati mwingine yanaumiza sana huwa mengine yanatupata kwa sababu maalumu na wakati mwingine Mungu anaweza kuyatumia hayo ili kujitwalia Utukufu.

- Ni kweli yanaweza yakawa ni maumivu makali sana ambayo mtu unapitia au anayapitia lakini ninachojua ni kwamba Mungu ni mwaminifu sana hata katika jambo baya ambalo unalipata au katika maumivu na majeraha ya ndani unayopitia bado unaweza kufanikiwa na Mungu akayatumia hayo kwa ajili ya Utukufu wake

- Upofu wa huyu ndugu najua haukuwa kitu chepesi, kuna mambo alitamani kuyaona na inawezekana ilikuwa inamuuma sana ndani yake lakini kumbe eti kupitia hali hiyo **Kuna Udhihirisho wa kazi za Mungu ambao unatakiwa utokee kupitia hali yake aliyonayo**

- Inawezekana hata wazazi wake waliumia sana kwa hali aliyokuwa nayo huyu mtoto wao, na inawezekana kabisa kuna watu wengine waliokuwa na mawazo kama ya wanafunzi wa Yesu kuwa ni sababu ya dhambi na ndio maana huyu ndugu akazaliwa katika hali ya upofu, lakini si kweli.

- Wimbo namba 117 katika kitabu cha Tenzi za Rohoni unaitwa *Tufani Inapovuma*, ukifika beti la Tatu la wimbo huo kuna maneno yafuatayo;

*Adui wakiniudhi
Nami nikisumbuka,
Mungu atavigeuza
Vyote viwe Baraka.*

- Kwa hiyo basi ni muhimu kujua ni kweli kabisa kuna wakati tunapitia maumivu na wakati mwingine tunapitia mambo ambayo kwa ahli ya kawaida yanaumiza sana ila mwisho wa siku ni muhimu kumhitaji Mungu ageuze kila lililo baya na ambalo adui amelikusudia ili kufanya kuwa la Baraka.

- *Inawezekana kabisa watu wanashangaa kwamba una shida gani mpaka leo huoi au huolewi, au wanatamani kujua na wanadadisi kwanini wewe tundo hujafanikiwa, au kwanini changamoto kila siku zinakukabili wewe, na tena kwanini hamjapata mtoto japo mmekaa kwenye ndoa kwa muda mrefu na hayo yote yanakuletea maumivu makali sana moyoni mwako*

- *ila nikutie moyo ya kwamba Kama Yesu alivyopita akamwona kipofu hakika atapita kwenye maisha yako na wewe na ataliona tatizo ambalo wengi walihisi ni dhambi na wengi walihisi ni mkosi na wengi walihisi kuna shida kwako lakini YESU ATAITUMIA HIYO SHIDA na na hayo maumivu kwa ajili ya kuonesha kazi za Mungu na udhihirisho wake.*

- 3. *Tamani sana kujua na kuwa na ufahamu na Maarifa juu ya masuala ya uponyaji wa ndani lakini pia hata mambo mengine unayotaka kuyafanya ya kimwili na kiroho.*

- Ili uweze kuwa na ufahamu au maarifa juu ya masuala ya uponyaji wa ndani ni muhimu kuwa na kiu na hamu ya kutaka sana kujua juu ya suala hili na namna linavyofanyika katika kila hatua au watu mbalimbali unaokutana nao.

- Kwa hiyo cha kuhitaji sana ni maarifa na unayapata kwa kutaka na kuwa na mzigo wa kutaka kujua hilo na kulielewa kwa undani sana.

© ⁸ Basi jirani zake, na wale waliomwona zamani kuwa ni mwombaji, wakasema, Je! Huyu siye yule aliyekuwa akiketi na kuomba? ⁹ Wengine wakasema, Ndiye. Wengine wakasema, La, lakini amefanana naye. Yeye mwenyewe alisema, Mimi ndiye. ¹⁰ Basi wakamwambia, Macho yako yalifumbuliwaje?

- **¹¹ Yeye akajibu, Mtu yule aitwaye Yesu alifanya tope, akanipaka macho akaniambia, Nenda Siloamu ukanawe; basi nikaenda na kunawa, nikapata kuona. ¹² Wakamwambia, Yuko wapi huyo? Akasema, Mimi sijui.....**

- Maswali waliyouliza hawa jirani na wale waliokuwa wanamjua huyu jamaa ni maswali muhimu na kuyaangalia kwa umakini sana maana kuna kitu cha kujifunza ndani yake mpendwa wangu, hebu tuyaangalie tena haya maswali kwa umakini.

- ◎¹⁰ **Basi wakamwambia, Macho yako yalifumbuliwaje?..... Wakamwambia, Yuko wapi huyo?....**
- ◎ Ukisoma hayo maswali kuna mambo kadhaa unayapata ambayo ni muhimu sana kuyaelewa kwa undani, nilipokuwa natafakari mistari hii niliwaza mambo kadhaa;

- Inawezekana siku nyingi sana walitamani huyu ndugu awe anaona na inawezekana walitaka hata kujaribu kumsaidia lakini hawakuwa na ufahamu ambao unahitaji na ambao Yesu alikuwa nao.



- Inawezekana pia walitaka wajue namna ya kufanywa jambo hili ili nao wafungue yamkini “clinic” ya kuwasaidia wagonjwa.

- Kwa hiyo ni muhimu sana kuwa na ufahamu wa jambo au kitu unachotaka kukishughulikia haswa unapokuwa unashughulika na suala linalohusu majeraha au maumivu ya ndani kwako binafsi au kwa mtu mwingine.

- Tafuta ufahamu sahihi, wekeza muda kwenye kujua kwa undani juu ya suala la uponyaji wa ndani, chunguza maandiko na upate muda wa kuomba hekima na maarifa ya kushughulika na suala la uponyaji wa ndani,

- Hii itakusaidia wewe binafsi kuhakikisha unasogea kutoka kiwango kimoja hadi kiwango kingine na itakupa Nguvu sana katika kushughulika na masuala ya uponyaji wa ndani.

Mambo ya msingi kufahamu na kuwa na maarifa nayo juu ya Uponyaji wa ndani.

Mambo tutakayoyatazama ni kama ifuatavyo:

- Vyanzo mbalimbali vya majeraha au maumivu ya ndani.
- Namna ya kushughulika na majeraha ya ndani ili kuleta uponyaji wa ndani kulingana na chanzo cha majeraha husika.

- **Majeraha yanayozaliwa kutokana na mtu kukubali kuamini jambo ambalo linaumiza na linachoma hata kama hana uhakika nalo.**

- Hii imewaumiza wengi sana katika maisha yao, **anasikia jambo analipa nafasi kwenye moyo na kisha analiamini hata kama hana uhakika nalo**, kisha linageuka kuwa maumivu makali sana na majeraha ndani ya moyo wake na maisha yake.

● **Mwanzo 37:13-20, 31-35 inasema hivi;**

**13 Israeli akamwambia Yusufu, Je! Ndugu
zako hawachungi kondoo katika
Shekemu? Njoo, nikutume kwao.
Akamwambia, Mimi hapa. 14
Akamwambia, Enenda, basi, ukaone
kama ndugu zako hawajambo, na kundi
nalo li salama, ukaniletee habari. Basi
akampeleka kutoka bonde la Hebroni,
akafika Shekemu.**

- 15 Mtu mmoja akamkuta, naye alikuwa anazunguka-zunguka katika nyika; yule mtu akamwuliza, akisema, Unatafuta nini? 16 Akasema, Nawatafuta ndugu zangu; tafadhali uniambie mahali wanakochunga. 17 Yule mtu akasema, Wametoka hapa, maana niliwasikia wakisema, Twendeni Dothani. Basi Yusufu akawafuata ndugu zake akawakuta huko Dothani.

- 18 Wakamwona toka mbali, na kabla hajawakaribia, wakafanya shauri juu yake ili wamwue. 19 Wakasemezana wao kwa wao, Tazama, yule bwana wa ndoto anakuja. 20 Haya, twende, tukamwue na kumtupa katika birika mojawapo, nasi tutasema, Mnyama mkali amemla; kisha tutaona zitakuwaje ndoto zake.....

³¹ Wakaitwaa kanzu ya Yusufu, wakachinja mwana-mbuzi, na kuichovya kanzu katika damu. ³² Wakaenda nayo ile kanzu ndefu, wakamletea baba yao, wakasema, Tumeona hii; basi, utambue kama kanzu hii ni ya mwanao, ama siyo. ³³ Akaitambua, akasema, Ndiyo kanzu ya mwanangu, mnyama mkali amemla; bila shaka Yusufu ameraruliwa.

**34 Yakobo akararua mavazi yake,
akajivika gunia viunoni, na kumlilia
mwanawe siku nyingi. 35 Wanawe
wote, na binti zake wote, wakaondoka
wamtulize, lakini akakataa kutulizwa,
akasema, La! Nitamshukia
mwanangu, nikisikitika, hata kuzimu.
Baba yake akamlilia.**

- Mara nyingi huwa kuna taarifa tunaletewa na watu au tunazona mahali au kuzisoma na kuziamini kisha zinaleta madhara kwenye maisha yetu na ndio maana **sio kila kitu unakipa moyo vingine inabidi uishie kuvipa masikio tu.**

⦿ Hesabu 13:27-33, **14:1-10** tunasoma hivi;

27 Wakamwambia wakasema, Tulifika nchi ile uliyotutuma, na hakika yake, ni nchi yenye wingi wa maziwa na asali, na haya ndiyo matunda yake. **28** Lakini watu wanaokaa katika nchi ile ni hodari, na miji yao ina maboma, nayo ni makubwa sana; na pamoja na hayo tuliwaona wana wa Anaki huko.

29 Amaleki anakaa katika nchi ya Negebu; na Mhiti, na Myebusi, na Mwamori wanakaa katika milima, na Mkanaani anakaa karibu na bahari; na kando ya ukingo wa Yordani. 30 Kalebu akawatuliza watu mbele ya Musa, akasema, Na tupande mara, tukaitamalaki; maana twaweza kushinda bila shaka.

- 31 Bali wale watu waliopanda pamoja naye wakasema, Hatuwezi kupanda tupigane na watu hawa; kwa maana wana nguvu kuliko sisi. 32 Wakawaletea wana wa Israeli habari mbaya ya ile nchi waliyoipeleleza, wakasema, Ile nchi tuliyopita kati yake ili kuipeleleza, ni nchi inayowala watu wanaoikaa; na watu wote tuliowaona ndani yake ni watu warefu mno. 33 Kisha, huko tuliwaona Wanefili, wana wa Anaki, waliotoka kwa hao Wanefili; tukajiona nafsi zetu kuwa kama mapanzi; nao ndivyo walivyotuona sisi.....

¹ Mkutano wote wakapaza sauti zao wakalia; watu wakatoka machozi usiku ule. ² Kisha wana wa Israeli wote wakamnung'unikia Musa na Haruni; mkutano wote wakawaambia, Ingekuwa heri kama tungalikufa katika nchi ya Misri, au, ingekuwa heri kama tungalikufa katika jangwa hili.

³ Mbona Bwana anatuleta mpaka nchi hii ili tuanguke kwa upanga? Wake zetu na watoto wetu watakuwa mateka; je! Si afadhali turudi Misri? ⁴ Wakaambiana, Na tumweke mtu mmoja awe akida, tukarudi Misri. ⁵ Ndipo Musa na Haruni wakaanguka kifudifudi mbele ya mkutano wa kusanyiko la wana wa Israeli.

- ⑥ ⁶ Na Yoshua mwana wa Nuni, na Kalebu mwana wa Yefune, waliokuwa miongoni mwao walioipeleleza nchi, wakararua nguo zao; ⁷ wakanena na mkutano wote wa wana wa Israeli wakasema, Nchi ile tuliyopita kati yake ili kuipeleleza, ni nchi njema mno ya ajabu. ⁸ Ikiwa Bwana anatufurahia, atatuingiza katika nchi hii atupe iwe yetu, nayo ni nchi yenye wingi wa maziwa na asali.

⁹ Lakini msimwasi Bwana, wala msiwaogope wale wenyeji wa nchi, maana wao ni chakula kwetu; uvuli uliokuwa juu yao umeondolewa, naye Bwana yu pamoja nasi; msiwaogope.

¹⁰ Lakini mkutano wote wakaamuru wapigwe kwa mawe. Ndipo utukufu wa Bwana ukaonekana katika hema ya kukutania, mbele ya wana wa Israeli wote.

Kuna wakati kuna taarifa au mambo au mafundisho au hadithi au historia tunaletewa katika maisha yetu ambayo ukishatoa nafasi tu kwenye moyo wako unajikuta zinakutesa na unaumia sana, unasikia mwingine amekusema vibaya au amekusingizia jambo unajikuta unaumia sana ni kwa sababu tu umeweka moyoni sana na unaumizwa.

NAMNA YA KUSHUGHULIKIA:

- ◎ Unachotakiwa ni **Kujifunza kuyachunguza mambo kwa undani kabla ya kuyaamini na kuyachukua kisha yakakutesa.**

● **Mwanzo 37:33 imeandikwa;**

³³ Akaitambua, akasema, Ndiyo kanzu ya mwanangu, mnyama mkali amemla; bila shaka Yusufu ameraruliwa. ³⁴ Yakobo akararua mavazi yake, akajivika gunia viunoni, na kumlilia mwanawe siku nyingi. ³⁵ Wanawe wote, na binti zake wote, wakaondoka wamtulize, lakini akakataa kutulizwa, akasema, La! Nitamshukia mwanangu, nikisikitika, hata kuzimu. Baba yake akamlilia.

- ◎ **Ni muhimu sana kuchunguza mambo kabla ya kuyaamini na kuyabeba kisha ukakuta yanakutesa pasipo sababu yoyote.**

● **1 Wafalme 3:16-21 imeandikwa;**

¹⁶ Ndipo wanawake wawili, makahaba, walimwendea mfalme, wakasimama mbele yake. ¹⁷ Na mwanamke mmoja akasema, Ee bwana wangu, mimi na mwanamke huyu tunakaa katika nyumba moja; nami nalizaa nilipokuwa pamoja naye nyumbani.

¹⁸ Kisha, siku ya tatu baada ya kuzaa kwangu, ikawa mwanamke huyu naye akazaa; na sisi tulikuwa pamoja; hapakuwa na mtu mwingine pamoja nasi nyumbani, isipokuwa sisi wawili tu. ¹⁹ Na mtoto wa mwanamke huyu akafa usiku, maana alimlalia.

²⁰ Akaondoka kati ya usiku, akamwondoa mtoto wangu ubavuni pangu, mimi mjakazi wako nilipokuwa usingizini, akamweka kifuani pake, na mtoto wake mwenyewe, aliyekuwa amekufa, akamweka kifuani pangu. ²¹ Nilipoondoka asubuhi nimnyonyeshe mtoto wangu, kumbe? Amekufa. Hata asubuhi nilipomtazama sana, kumbe! Siye mtoto wangu niliyemzaa.

- Huyu mama angeweza kulia usiku ule kwa ajili ya kufiwa na mwanawe, lakini alisubiri asubuhi akamtazama sana akamchunguza akagundua sio wa kwake, kuna mambo yanatumiza lakini sio ya kwetu kabisa.

2. Majeraha ya ndani yanayotokana na kufanyiwa jambo hasa lililo baya na mtu usiyemtarajia.

Kuna mambo mengine yanaumiza si kwa sababu ni mabaya sana ila ni kwa sababu hukutegemea kutendewa na aliyekutendea jambo hilo, kwa hiyo maumivu yake ni kwa sababu ya aina ya mtu aliyekufanyia jambo hilo kwenye maisha yako.

◎ **Luka 10:30-34** inasema hivi;

³⁰ Yesu akajibu akasema, Mtu mmoja alishuka toka Yerusalemu kwenda Yeriko, akaangukia kati ya wanyang'anyi; wakamvua nguo, wakamtia jeraha, wakaenda zao, wakimwacha karibu ya kufa. ³¹ Kwa nasibu kuhani mmoja alishuka kwa njia ile; na alipomwona alipita kando.

³² Na Mlawi vivyo hivyo, alipofika pale
akamwona, akapita kando. ³³ **Lakini,**
Msamaria mmoja katika kusafiri
kwake alifika hapo alipo; na
alipomwona alimhurumia, ³⁴
akakaribia, akamfunga jeraha zake,
akizitia mafuta na divai;
akampandisha juu ya mnyama wake,
akampeleka mpaka nyumba ya
wageni, akamtunza.

Inawezekana kuna watu hukutegemea watakuja kukuacha kwenye hali mbaya kwenye maisha, na hukutegemea wangekuacha kwenye hali hiyo na wamekugeuka na kukuacha kabisa.

● **Yeremia 30:14** tunasoma hivi;

**14 Wote wakupendao wamekusahau;
hawakutafuti; maana nimekujeruhi
kwa jeraha ya adui, kwa adhabu ya
mtu mkatili; kwa sababu ya ukubwa
wa uovu wako, kwa sababu dhambi
zako zilikuwa zimeongezeka.**

Zaburi 41:9 inasema hivi;

**⁹ Msiri wangu tena niliyemtumaini,
Aliyekula chakula changu,
Ameniinulia kisigino chake.**

- Mzaburi anatuonesha kuwa kuna wakati ambao wale watu uliowategemea na uliwaamini wanaweza kukugeuka kabisa na ukajikuta unapata shida kubwa ya maumivu kwenye maisha yako.

NAMNA YA KUSHUGHULIKIA:

- ◎ Katika hali hii jifunze kuamini na kuiambia nafsi yako kwamba
**TUNAWAHITAJI WATU LAKINI
TUNAMTEGEMEA MUNGU PEKE
YAKE.**

- Kwa hali ya kawaida hatuwezi kuendesha maisha peke yetu kana kwamba duniani hakuna watu, lakini lazima tujue kuwa tunawahitaji watu lakini tunamtegemea Mungu, kiasi kwamba hata watu wote wakikuacha na wakawa mbali nawe na kukugeuka lakini kwa Bwana bado liko tumaini kila siku na kila saa.

◎ Mathayo 28:18-20 imeandikwa hivi;

Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. ¹⁹ Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; ²⁰ na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, **mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.**

- Yesu pekee ndiye rafiki wa kweli hakika anaweza kuwa nasi katika mazingira yote, usiogope ukiachwa na wanadamu maana nao wanachoka nao wanazimia njiani na wanakosa stamina wakati mwingine lakini kuwa na Yesu ni bora na kumtegemea yeye.

● Isaya 49:14-16 imeandikwa;

14 Bali Sayuni alisema, YEHOVA ameniacha, Bwana amenisahau. ¹⁵ Je! Mwanamke aweza kumsahau mtoto wake anyonyaye, hata asimhurumie mwana wa tumbo lake? Naam, hawa waweza kusahau, lakini mimi sitakusahau wewe. ¹⁶ Tazama, nimekuchora katika vitanga vya mikono yangu; kuta zako ziko mbele zangu daima.



Mwl. Samwel Mkumbo



+255 764 190 790



Mwl. Samwel Mkumbo



Mwl. Samwel Mkumbo



mkumbo.nuruministry